

Kikundi cha wafuga nyuki kutoka mtandao wa UMIZOMA, kijiji cha Nyali

**Taarifa na katibu wa mtandao UMIZOMA,
Ndg. Anthon Method Saanane.**

UMIZOMA ni Uhifadhi wa Misitu Zombo na Masanza. Mtandao huu ulianzishwa tarehe 14-07-2011, ukiwa na wanachama waanzilishi 35 kutoka vijiji vinne, kata mbili ambao ni wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji na wenyeviti wa vijiji hivyo vya Nyali, D/lsanga, Chabima na Munisagara.

Tangu kuanza kwa huu mtandao kumekuwa kukifanyika shughuli mbalimbali za vikundi katika hivyo vijiji vya mtandao. Shughuli hizo ni pamoja na uhifadhi wa misitu ya asili, shughuli nyingine zilizokuwa zikifanywa na wanachama wa vikundi vya UMIZOMA ni elimu ya uhamasishaji kwa jamii juu ya uhifadhi wa misitu yao pamoja na kutambua umuhimu wake. Pia kumekuwa kikitolewa elimu mbalimbali za misitu pamoja na shughuli ambazo vikundi vinapaswa kushughulika katika misitu yetu.

Miongoni mwa elimu hizo ni pamoja na ufgajji wa nyuki na tayari kijiji kimoja cha mtandao ambacho ni Chabima

kimeshapata elimu hiyo na kijiji kingine cha Nyali kinataraja kupata elimu hiyo ya ufgajji wa nyuki hivi punde. Kijiji hiki kilikuwa na wafuga nyuki tangu zamani ila walikuwa wakitumia njia za asili ambazo ni ufgajji kwa magome ya miti. Lakini kwa bahati nzuri kikundi cha ufgajji cha Nyali kimepokea mizinga mitano ya kisasa mnamo tarehe 03-04-2012. Hivyo kikundi kinatoa shukrani kwa MJUMITA na kinategemea kuwa na ufgajji endelevu na wenyе mafanikio.

